## Maswali

1. Mbona Yesu alichagua hao wanafunzi kumi na mbili?
2. Yesu alifanya nini kabla hajachagua hao wanafunzi?
3. Wanafunzi gani wanne walikuwa wavuvi?
4. Walifanya nini Yesu alipowambia wamfuate?
5. Ni mwanafunzi yupi ana jina la Kiyunani?
6. Mathayo alifanya kazi gani?
7. Mathayo alipoitwa na Yesu alifanya nini?
8. Yuda Iskariote alifanya makosa gani?
9. Wanafunzi walifanya nini Yesu alipoenda mbinguni?
10. Wanafunzi watafanya nini wakati Yesu atarudi.

## Majibu

1. Yesu alichagua wanafunzi ili wamsaidie kazi ya Mungu tena waendeleze hiyo kazi baada ya yeye kwenda mbinguni.
2. Yesu aliomba usiku kucha kabla ya kuchagua wanafunzi.
3. Petro, Andrea, Yakobo na Yohana walikuwa wavuvi.
4. Waliacha nyavu zao na kufuata Yesu.
5. Filipo ana jina la Kiyunani.
6. Mathayo alikuwa mtosha ushuru.
7. Mathayo aliacha kila kitu na akamfuata.
8. Yuda Iskariote aliiba pesa tena alimsaliti Yesu.
9. Walihubiri injili, waliandika habari ya Yesu, walisimamisha makanisa waliandika barua, wengi wao waliteswa na wengine waliuwawa.
10. Yesu atawafufua kutoka kwa wafu. Watasaidia Yesu kutawala, mataifa.

**SHULE YA JUMAPILI YA CBM**

**Awamu ya 1 Mwaka wa 2**

# 33 Yesu anachagua wanafunzi wake

## Marejeo

Mathayo 4:18—22 tena 9:9—10; Luka 6:12—16

## Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba vile Yesu alichagua wanafunzi wake, waliacha yote na kumfuata. Yesu anataka tuwe wanafunzi wake.

## Maneno maalum

1. Kazi ya kufanya + funza + miujiza + watu 12 kusaidia.
2. Wanafunzi + linda + soma + sikiliza.
3. Chagua vizuri + Yesu aliomba.
4. Wavuvi 4 + nifuate + Petro + Yakobo + Yohana + Andrea.
5. Filipo + Bethsaida + jina la Kiyunani.
6. Mathayo + mtosha ushuru + wacha yote.
7. Yuda Iskariote + alilinda mfuko wa pesa + alisaliti Yesu.
8. Wanafunzi wengine + nao walihubiri + Ufalme wa Mungu.
9. Andika injili + anzisha makanisa + barua katika Agano Jipya.
10. Umia + kufa ajili ya Yesu + Ufufuo.

**33.1** Yesu alikuwa na kazi nyingi ya kufanyia Mungu. Lazima afundishe watu wote juu ya ufalme wa Mungu. Lazima awaonyeshe vile wanamfuata Mungu na kumfanyia yanayompendeza. Alifanya miujiza mingi. Miujiza ilionyesha watu kwamba Mungu alikuwa amempa uwezo usio wa kawaida. Yesu alikuwa na kazi muhimu ya kufanya. Alikuwa na miaka mitatu tu kufanya kazi hii yote. Akachagua watu kumi na mbili kumsaidia.

**33.2** Hao watu kumi na mbili waliitwa wanafunzi. Mwanafunzi ni mtu mwenye ako anafunzwa au kuongozwa. Yesu aliongoza hawa wanafunzi kufanya kazi ya Mungu. Aliwafundisha ili waendeleze kazi ya Mungu baada ya yeye kwenda kuishi na Mungu mbinguni. Wanafunzi walisikiliza kila kitu alichosema. Waliangalia vile alifanya miujiza. Walijifunza kutoka kwa Yesu ili waendelee kama ameenda. Yesu alifundisha wanafunzi kuhusu Ufalme wa Mungu. Wakati mwingine Yesu alituma wanafunzu wafunze na wafanye miujiza. Aliwatuma washugulike na kazi ya Mungu.

**33.3** Yesu alijua kwamba ni jambo la maana kuchagua watu wazuri kumsaidia. Alitaka watu wenye wangefanya kazi ya Mungu vizuri baada ya yeye kuenda mbinguni. Usiku kucha Yesu aliomba Mungu. Aliomba Mungu amusaidie achague watu wazuri. Mungu alimsaidia kuchagua watu wazuri. Hao wanafunzi walifanya kazi ya Mungu vizuri sana. Walifundisha watu ulimwengu mzima juu ya Yesu na juu ya Ufalme wa Mungu. Ndio sababu hata sisi tunaendelea kusoma juu ya hayo hata sasa.

**33.4** Yesu alichagua wavuvi wanne kama wanafunzi wake. Petro, Andrea, Yakobo na Yohana walikuwa wavuvi. Siku moja Yesu akawambia “nifuate.” Hao wavuvi wanne waliacha nyavu zao na wakamfuata. Wakawa wanafunzi wake. Mda mwingi Petro alikuwa kiongozi wao. Alikuwa mjasiri tena mkarimu. Wakati mwingine Petro alikuwa na haraka. Yeye ndiye alikuwa mwanafunzi wa kwanza kuamini kwamba Yesu ni mwana wa Mungu. Petro, Yakobo na Yohana walikuwa marafiki wa karibu wa Yesu. Yesu alimpenda Yohana sana.



**33.5** Filipo alikuwa mwanafunzi wa kwanza kukutana na Yesu. Filipo aliishi Bethsaida ukingoni mwa bahari ya Galilaya. Jina lake ni la Kiyunani na labda alizungumza Kiyunani. Wakati Wayunani walitaka kuzungumza na Yesu, waliuliza Filipo awasaidie.



**33.6** Mathayo alikuwa mtosha ushuru. Yesu alimuita Mathayo wakati alikuwa amekaa kwa dawati yake akikusanya ushuru. Mathayo aliwacha kila kitu na kumfuata Yesu. Alifurahi kwa sababu Yesu alimchagua yeye kama mwanafunzi. Aliwafanyia marafiki wake karamu kubwa.

**33.7** Yesu alichagua Yuda Iskariote kuwa mwanafunzi wake. Yuda alifanya kazi moja kama wanafunzi wengine. Alisaidia kwa kufundisha na kuponya. Yuda alikuwa akiweka mfuko wa pesa ya wanafunzi wote. Lakini alikuwa mwizi. Aliiba pesa kutoka kwa huo mfuko. Yuda alimsaliti Yesu kwa vipande thelathini vya fedha. Baadaye alisikitika kwa kitendo alichokifanya- alirudishia makuhani hizo pesa na akajinyonga.

**33.8** Hatujaambiwa sana kuhusu wanafunzi wengine. Tunajua walifanya bidii sana na kusaidia Yesu. Baada ya Yesu kwenda mbinguni, waliendelea na kazi ya Mungu. Waliambia kila mtu habari ya Yesu. Waliambia watu vile Yesu alikaa maisha isiyo na mawaa na akafa kwa ajili ya dhambi zetu. Waliambia watu kwamba wakati moja Yesu atarudi kutoka mbinguni. Yesu atarudi hapa duniani. Atawafufua wafu. Atasimamisha Ufalme wa Mungu hapa duniani. Atatawala ulimwengu mzima milele. Hii ndio injili wanafunzi walihubiria watu ulimwenguni kote.

**33.9** Baadhi ya wanafunzi waliandika mambo yaliyofanywa na Yesu. Tunasoma habari hii ya Yesu katika injili walizoziandika. Baadhi ya wanafunzi walisafiri na kusimamisha makanisa pahali tofauti tofauti. Baadhi yao waliandikia hizo kanisa barua. Tunasoma hizi barua katika Agano Jipya.

**33.10** Baadhi ya hao wanafunzi waliteswa vibaya. Baadhi yao walikufa kwa ajili ya Yesu. Yesu atakaporudi hapa duniani, atawafufua kutoka kwa wafu. Watamsaidia kutawala ulimwengu katika Ufalme wa Mungu.